*Mulika, Na. 42 (2), 164-183*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Ufundishaji na Ujifunzaji wa Somo la Kiswahili Unaozingatia Stadi ya Tafakuri Tunduizi: Mifano kutoka Shule Teule za Sekondari Wilayani Nyagatare

*Laurien Tuyishimire*[1]
Chuo Kikuu cha Rwanda
na
*Wallace Kapele Mlaga*[2]
Chuo Kikuu cha Rwanda

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na42t2.2

**Ikisiri**

Makala haya yanajadili kuhusu ufundishaji na tathmini ya masomo ambayo inazingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Makala yanaongozwa na malengo mahususi mawili: Mosi, ni kujadili namna walimu wa Kiswahili wanavyofundisha na kutathmini masomo yao kwa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Pili, ni kubainisha changamoto zinazowakabili walimu wa Kiswahili wakati wa kufundisha na kutathmini masomo yao wakizingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Data za makala haya zimekusanywa kwa kutumia njia mbili ambazo ni mahojiano na uchambuzi matini. Data zilizokusanywa zilichambuliwa kimaelezo kwa kuongozwa na Nadharia ya Ujengaji. Matokeo ya utafiti yamebainisha kwamba, walimu wa Kiswahili wanashindwa kufundisha na kutathmini kwa ukamilifu masomo wanayofundisha kwa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Hii ni kutokana na kutumia malengo ya ujifunzaji ya kiwango cha chini katika Taksonomia ya Bloom na kuuliza maswali ambayo yanamtaka mwanafunzi kukariri kile alichosoma badala ya kukihusisha na hali halisi ya maisha. Aidha Makala yanabainisha sababu za kuwapo kwa dosari na kutoa mapendekezo ya namna ya kukabiliana na dosari hii.

## 1.0 Utangulizi

Lengo la msingi la ufundishaji na ujifunzaji wa somo lolote ni kumwezesha mwanafunzi kupata uwezo unaohitajika katika mazingira tofauti ya utatuzi wa tatizo (Ndihokubwayo, Habiyeremye na Rukundo, 2019). Kwa mantiki hiyo, mwanafunzi anatakiwa kujengewa mazingira yanayomsaidia kuwa na uwezo wa kutatua matatizo ya kimaisha yanayoweza kumkabili mwanajamii yoyote. Uwezo, kwa ujumla, unamaanisha hali ya mtu kuweza kufanya kitendo fulani kwa kiwango kilichowekwa. Katika muktadha wa darasa, uwezo unahusiana na hali ya mwanafunzi kutumia muunganiko sahihi wa maarifa, stadi, maadili na mitazamo ili

[1] Baruapepe: tulaurien@gmail.com
[2] Baruapepe: wamlaga@gmail.com

kufanikisha kazi anayopewa (REB, 2015a). Maelezo haya yanamaanisha kwamba mwanafunzi anaweza kutumia kile alichojifunza darasani kukabiliana na changamoto yoyote inayoweza kumkabili. Kwa mfano, mwanafunzi anaweza kuandika barua rasmi kwa ajili ya kuomba huduma anayohitaji badala ya kuishia tu kutaja sifa bainifu za barua na sehemu zake. Aidha, mwanafunzi anaweza kuandaa hotuba itakayotolewa katika sherehe au mkutano kuliko kuishia kueleza maana, sifa, na sehemu tu za hotuba.

Ili mwanafunzi aweze kufanikisha haya, analazimika kuwa na umilisi wa stadi za karne ya 21. Kwa mantiki hiyo, stadi za karne ya 21 zinapaswa kujumuishwa kwa kila somo linalofundishwa (Kaufman, 2013). Aidha, umilisi wa stadi za karne ya 21 utawasaidia pia wanafunzi kujiandaa kwa elimu ya juu (Alismail na McGuire, 2015 katika Bakhshandeh, 2021). Stadi za karne ya 21 ni pamoja na tafakuri bunifu, tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatizo, kufanya maamuzi, mawasiliano katika lugha rasmi, Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha na ujifunzaji wa muda mrefu (REB, 2015a).

Ili kufundisha stadi za karne ya 21, nchi mbalimbali duniani zilibadilisha mitaala yao ya elimu na kuanza kutekeleza mtaala unaoegemea katika uwezo (Chu, Reynolds, Tavares, Notari na Lee, 2017). Mtaala huu unarejelewa pia kwa majina tofauti katika nchi mbalimbali. Kwa baadhi ya nchi unarejelewa kama mtaala unaoegemea katika ujuzi au mtaala unaoegemea katika umilisi. Nchini Rwanda wanaurejelea kama mtaala unaoegemea katika uwezo (Tuyishimire, 2022).

Kwa mfano, malengo ya kubadilisha maudhui ya mtaala katika nchi za bara la Afrika yalikuwa kuyafanya yafae zaidi sio tu katika kiwango cha kitaifa na kimataifa, bali pia yaendane na uwezo unaohitajika katika mazingira ya kazi (Muraraneza, Mtshali na Mukamana, 2017). Ili kufanikisha haya, ufundishaji wa stadi ya tafakuri tunduizi ulitiliwa mkazo (Nsengimana, 2021).

Morale (2011) akirejelewa na Mashaza (2017) anaeleza kwamba stadi ya tafakuri tunduizi inamsaidia mwanafunzi kufikiria kwa mapana na kimantiki juu ya changamoto lukuki katika hali zote za maisha. Mwanafunzi mwenye tafakuri tunduizi huchagua hoja zinazofaa kwa ajili ya kutatua matatizo yanayomkabili. Baadhi ya matatizo hayo ni kama vile ongezeko la joto duniani, Janga la Uviko 19, Ugonjwa wa Ebola, na matatizo mengine.

Isitoshe, stadi ya tafakuri tunduizi inafanikisha utekelezaji wa stadi nyingine za karne ya 21. Lau (2011) anaeleza kwamba stadi ya tafakuri tunduizi inasaidia tafakuri bunifu katika kuendeleza na kutathmini hoja au mawazo mapya yanayobuniwa ili kutatua tatizo. Stadi ya tafakuri tunduizi inasaidia sio tu kutambua tatizo bali pia kutathmini taarifa, hoja na matukio yote yanayochangia katika utatuzi wake (Sünbül na Kurnaz, 2016).

Aidha, stadi ya tafakuri tunduizi inachangia katika ukuzaji wa stadi za mawasiliano. Stadi ya tafakuri tunduizi inasaidia katika uchaguzi wa msamiati faafu wa kutumia katika mchakato wa mawasiliano na namna msamiati huo unavyopaswa kutumiwa (Paul na Elder, 2007 katika Tuyishimire, 2022).

Mtaala unaotumiwa nchini Rwanda unaweka mkazo kwenye ufundishaji wa tafakuri tunduizi kwa kila somo ili kuwasaidia wanafunzi kuwa na umilisi wa stadi za karne ya 21. Hii ina maana kwamba ufundishaji wa tafakuri tunduizi katika somo la Kiswahili utawasaidia wanafunzi kuwa na umilisi wa stadi za karne ya 21 ikiwa ni pamoja kuwasiliana kwa ufanisi. Kwa hiyo, wanafunzi wa Kiswahili wataweza kushiriki na kufanikisha shughuli mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa zinazohitaji matumizi ya Kiswahili. Aidha, wataweza kupata ajira mbalimbali kama vile tafsiri na ukalimani, uandishi na utangazaji habari na utoaji wa huduma kwa wateja (REB, 2015). Hivyo basi, njia mojawapo ya kuwaandaa wahitimu wa Kiswahili wenye uwezo wa kushindana kwenye soko la ajira na kuwawezesha kufanya kazi kwa ufanisi ni kuwafundisha tafakuri tunduizi.

Hata hivyo, tafiti zinaonesha kwamba wahitimu wa viwango mbalimbali vya elimu wakiwamo wa vyuo vikuu wana kiwango cha chini cha tafakuri tunduizi (Schendel, 2015; Bakhshandeh, 2021). Sababu za msingi zinazowafanya wahitimu hawa kuwa na kiwango hiki ni kukosa misingi bora ya stadi ya tafakuri tunduizi katika shule za sekondari (Masduqi, 2011). Walimu wa shule za sekondari wanaonekana kutoielewa vema stadi ya tafakuri tunduizi na hivyo wanashindwa kuifundisha vizuri (Khalid, Bucheerei na Issah, 2021).

Licha ya hayo, Phan (2011) na Arum na Roska (2011) kama wanavyorejelewa na Schendel (2015) wanadokeza kwamba wanafunzi wanapofundishwa vizuri tafakuri tunduizi katika ngazi ya sekondari wanaendelea kuwa na kiwango kizuri cha stadi hii hata wanapofika vyuo vikuu. Isitoshe, Carrasco (2021) anaongezea kwamba ufundishaji wa stadi ya tafakuri tunduizi katika shule za sekondari utawanufaisha pia wanafunzi ambao hawatapata fursa ya kuendelea na elimu ya juu.

Maelezo haya yanatuchochea kujiuliza maswali mawili yafuatayo: Je, ni namna gani walimu wa Kiswahili wanafundisha na kutathmini masomo yao kwa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi? Changamoto zipi zinawakabili walimu wa Kiswahili wakati wa kufundisha na kutathmini masomo yao wakizingatia stadi ya tafakuri tunduizi? Majibu ya maswali haya yanatusaidia siyo tu kupata picha halisi ya namna walimu wanavyoandaa masomo yao na ufanyaji wa tathmini unaozingatia stadi ya tafakuri tunduizi bali pia namna mtaala unaoegemea katika uwezo unavyotekelezwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili. Kabla ya kujibu maswali haya, ni muhimu kujadili methodolojia na nadharia iliyoongoza utafiti huu.

## 2.0 Methodolojia na Nadharia ya Utafiti

Utafiti ulioibua makala haya ulikuwa wa kitaamuli na hivyo data zilizokusanywa zilikuwa za kitaamuli. Utafiti ulihusisha walimu wa Kiswahili kutoka shule mbili teule za sekondari katika Wilaya ya Nyagatare. Shule hizo ni G. S Rwimiyaga na G. S Nyagatare. Shule hizi ziliteuliwa kwa kutumia usampulishaji lengwa. Usampulishaji lengwa ni mchakato wa kuteua walengwa wa utafiti kimakusudi kwa kuwa wana taarifa muhimu zinazohusiana na suala linalotafitiwa (Cresswell, 2012). Shule hizi ziliteuliwa kwa kutumia vigezo vifuatavyo: Shule kuwa ya serikali na kuwa na mchepuo wa lugha ambapo Kiswahili ni somo la kutahiniwa katika mtihani wa taifa.

Kwa kuzingatia kwamba nchini Rwanda kila shule ya sekondari ina mwalimu mmoja tu wa Kiswahili, ilionekana kuwa ni vema kuongeza idadi ya walimu kwa ajili ya kupata data za kutosha. Kwa hiyo, utafiti huu ulihusisha pia walimu wawili wa Kiswahili kutoka shule jirani ambazo ni G. S Rwebare na G. S Nezerwa.

Data zilikusanywa maktabani kwa njia ya uchambuzi wa matini pamoja na mahojiano kwa ajili ya kufanikisha malengo ya utafiti. Lengo la kwanza kujadili namna walimu wa Kiswahili wanavyofundisha na kutathmini masomo yao kwa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Pili ni kubainisha changamoto zinazowakabili walimu wa Kiswahili wakati wa kufundisha na kutathmini masomo yao wakizingatia stadi ya tafakuri tunduizi.

Uchanganuzi wa matini mbalimbali ulitupatia picha kuhusu ufundishaji na tathmini ya somo la Kiswahili kwa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Aidha, katika tafiti tangulizi tulizozipitia, tulifanikiwa pia kubaini changamoto zinazowakabili walimu wa Kiswahili wakati wa kufundisha na kutathmini masomo yao wakizingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Hivyo, nyaraka za walimu wa Kiswahili zilichambuliwa ili kuchunguza namna wanavyoandaa masomo ya Kiswahili na tathmini yake kwa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Nyaraka za walimu wa Kiswahili zilizochambuliwa ni andalio la somo na mtihani wa Kiswahili wa muhula wa pili (2021-2022). Mtihani huu ulitolewa kwa wanafunzi wa kidato cha sita katika mchepuo wa lugha (*Literature in English*, Kinyarwanda na Kiswahili: LKK).
Mtihani huu uliandaliwa kwa kiwango cha Wilaya ya Nyagatare. Tulichambua mtihani wa kidato hiki kutokana na kwamba ni mtihani unaotoa fursa kwa wanafunzi kujiandaa na mtihani wa taifa wa kidato cha sita. Hii ina maana kwamba mtihani huu unazingatia taarifa nyingi kuhusu maarifa waliyoyapata katika silabasi ya Kiswahili ya shule za sekondari. Hivyo basi, mtihani huu ulitoa picha halisi ya namna stadi ya tafakuri tunduizi inavyozingatiwa katika tathmini.

Kwa upande wa mahojiano, walimu wanne wa Kiswahili walihojiwa. Lengo la kuwahoji walimu hawa, kwanza ni kutaka kupata taarifa kuhusu namna wanavyofundisha masomo yao kwa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Pili ni

kutaka kuelewa changamoto zinazowakabili walimu wa Kiswahili wakati wa kufundisha na kutathmini masomo yao wakizingatia stadi ya tafakuri tunduizi.

Katika uchambuzi na uwasilishaji wa data, misimbo tofauti ilitumiwa ili kutofautisha data zilizokusanywa. Msimbo wa A ulitumiwa kuwakilisha mwalimu wa Kiswahili katika shule ya kwanza, wakati ambapo msimbo wa B ulitumiwa kuwakilisha mwalimu wa shule ya pili. Aidha, msimbo wa CH ulitumiwa kuwakilisha mwalimu wa Kiswahili wa shule ya tatu na msimbo wa D kwa mwalimu wa shule ya nne.

Nadharia ya Ujengaji ilionekana kufaa katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za utafiti huu. Nadharia hii iliasisiwa na Piaget miaka ya 1980. Nadharia hii inaeleza namna watu wanavyojifunza na kupata maarifa kupitia tajriba zao (Olusegun, 2015). Pamoja na hayo, Nadharia ya Ujengaji inaweka mkazo katika ujifunzaji unaomshirikisha mwanafunzi kama kitovu cha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ambapo mwalimu anakuwa mwezeshaji. Mwanafunzi anapaswa kutumia maarifa yaliyopo na tajriba za maisha ya kila siku ili kupata maamuzi. Aidha, nadharia hii inasisitiza ushirikishanaji wa maarifa baina ya mwalimu na wanafunzi ambapo wote wana mamlaka katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji (Tam, 2000 katika Olusegun, 2015).

Pamoja na hayo, matumizi ya Nadharia ya Ujengaji katika ufundishaji huwasaidia wanafunzi kukuza stadi yao ya tafakuri tunduizi kama ifuatavyo: Wanafunzi huwa washiriki hai katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji; hivyo, huweza kuhamisha maarifa wanayojifunza darasani na kuyatumia katika maisha halisi. Aidha, Nadharia ya Ujengaji inaboresha stadi za kijamii na kimawasiliano kwa kutengeneza mazingira ya darasani yanayoweka mkazo kwenye ushirikiano na ubadilishanaji wa hoja (Olusegun, 2015).

Nadharia ya Ujengaji ina mihimili mingi (Ertmer na Newby, 2013; Olusegun, 2015). Makala haya yameegemezwa katika mihimili minne tu miongoni mwake: Mhimili wa kwanza ni kumuangalia mwanafuzi kama kitovu cha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mhimili huu ulitusadia kuchunguza iwapo walimu wa Kiswahili wanashirikisha wanafunzi katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji na hivyo kuwafanya kuwa kitovu cha mchakato wote.

Pili, kuwashirikisha wanafunzi katika ujenzi wa maarifa. Mhimili huu ulitusaidia kuchunguza iwapo walimu wa Kiswahili wanawasaidia wanafunzi kujenga maarifa yao wenyewe kutokana na kile wanachojifunza darasani, hivyo kuwawezesha kusaka maarifa zaidi kulingana na kile walichopewa.

Mhimili wa tatu ni tathmini inayopaswa kuweka mkazo kwenye uhamishaji wa maarifa na stadi. Mhimili huu ulitufaa katika utafiti huu kwa kuwa ulitusaidia

kuchunguza iwapo tathmini zinazotolewa kwa wanafunzi zinawasaidia kuhusisha masomo ya darasani na maisha halisi.

Mhimili wa nne ni ufundishaji unaoegemea katika utatuzi wa tatizo ambao ndio unaopaswa kuwa moyo wa ujifunzaji (Mashaza, 2017). Mhimili huu ulitusaidia kuchunguza iwapo walimu wa Kiswahili wanahusisha darasa na utatuzi wa tatizo unaojitokeza katika maisha halisi.

## 3.0 Matokeo ya Utafiti

Sehemu hii inaangazia matokeo ya utafiti. Kwa hiyo mjadala umeegemezwa katika utoaji wa majibu kwa maswali yafuatayo: Je, ni namna gani walimu wa Kiswahili wanafundisha na kutathmini masomo yao kwa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi? Changamoto zipi c zinawakabili walimu wa Kiswahili wakati wa kufundisha na kutathmini masomo yao wakizingatia stadi ya tafakuri tunduizi?


Hivyo basi, sehemu ya kwanza inajadili kuhusu ufundishaji wa tafakuri tunduizi. Sehemu ya pili inashughulika na tathmini ya somo la Kiswahili inayozingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Sehemu ya tatu inashughulika na changamoto za kufundisha na kutathmini somo la Kiswahili kwa kuzingatia tafakuri tunduizi. Sehemu ya mwisho ni hitimisho.

### 3.1 Ufundishaji wa Stadi ya Tafakuri Tunduizi

Tafakuri tunduizi ni stadi ambayo wanafunzi wanaweza kujifunza darasani kama stadi nyingine (Bean, 1996 katika Iakovos, 2011). Kwa hivyo, ni jukumu la walimu kutoa mazoezi mbalimbali kwa wanafunzi ili waweze kuwa na umilisi wa stadi hii.

Kincheloe (2004) akirejelewa na Sulaiman (2012) anatanabahisha kwamba walimu wanapaswa kuwa na uelewa kuhusu stadi ya tafakuri tunduizi ili waweze kuifundisha vizuri. Hii ina maana kwamba maarifa aliyonayo mwalimu yanamsaidia kutengeneza mikakati faafu ya ufundishaji. Mikakati hii inapaswa kuwahamasisha wanafunzi kuelewa, kugundua, kuchambua na kutathmini masuala mbalimbali ya kimaisha (Taba, 1966, katika Sulaiman, 2012).

Vdovina na Gaibisso (2013) wanasema kwamba ufundishaji wa tafakuri tunduizi unapaswa kuwa lengo la mwalimu la kila siku. Hii ina maana kwamba kila somo analoliandaa mwalimu, linapaswa kuonesha namna wanafunzi watakavyokuza stadi ya tafakuri tunduizi kuanzia malengo hadi tathmini ya somo, kama inavyoonekana kwenye mchoro ufuatao:




Malengo ya ujifunzaji humuongoza mwalimu katika uchaguzi wa mikakati mbalimbali anayotumia katika ufundishaji. Aidha, mikakati ya ufundishaji humsaidia mwalimu kuchagua aina ya maswali anayopaswa kuyatumia katika tathmini yake ya somo. Hivyo basi, andalio la somo linaonesha wazi kile kinachotendekea darasani. Hii ndio sababu utafiti huu ulijikita hasa katika uchunguzi wa namna walimu wa Kiswahili wanavyoandaa masomo yao kwa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi na tathmini ya masomo hayo.

Matokeo ya utafiti thuu yanaonesha kwamba baadhi ya walimu wa Kiswahili wanatatizika na ufundishaji wa tafakuri tunduizi. Jambo hili linajitokeza kuanzia namna wanavyoandaa malengo ya ujifunzaji.

Licha ya hivyo, wapo baadhi ya walimu ambao wanaonekana kuunda malengo ya ujifunzaji yanayowasaidia wanafunzi kuboresha stadi ya tafakuri tunduizi. Ifuatayo ni baadhi ya mifano ya malengo sahihi ya ujifunzaji kutoka kwa mwalimu mmojawapo:

1. Kwa kurejelea kifungu cha habari kitakachosomwa, wanafunzi watakuwa na uwezo wa kusoma matini ya "Usafi wa Mwili" na kujibu maswali ya ufahamu na kutumia msamiati katika sentensi kwa usahihi.
2. Kwa kurejelea kitabu cha mwanafunzi kidato cha tano, mwanafunzi, atakuwa na uwezo wa kusoma matini "Mdahalo kuhusu athari za mavazi ya Kisasa", kujibu maswali na kutumia msamiati mpya kuhusu mdahalo katika sentensi kwa usahihi (mwalimu, B).

**Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Malengo haya mawili yanaonesha wazi kile mwanafunzi atakachofanya mwishoni mwa somo kama matokeo ya ujifunzaji. Malengo haya pia yanaonesha namna wanafunzi watakavyotumia lugha lengwa katika mawasiliano. Kupitia mawasiliano na wenzao, watapata fursa ya kukuza stadi za tafakuri tunduizi ambazo ni kubuni na kutathmini hoja watakazozitoa au zitakazotolewa na wenzao.

Tofauti na walimu wachache walioonekana kuweza kuunda malengo sahihi ya ujifunzaji, walimu wengine walionekana sio tu kuunda malengo ya ujifunzaji yasiyo

sahihi bali pia waliunda malengo yasiyoweza kuwasaidia wanafunzi kukuza stadi yatafakuri tunduizi. Hii inadhihirishwa na mifano ifuatayo:

3. Baada ya somo hili, wanafunzi wataweza kufafanua na kueleza mifano ya matumizi na dhima ya fasihi katika jamii (mwalimu, D).

4. Kwa kutumia kielelezo cha fasihi, mwanafunzi ataeleza fasihi na tanzu zake (mwalimu, CH).

5. Baada ya somo hili, wanafunzi wataweza kutoa maana na kutumia nahau na misemo (mwalimu, CH).

**Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Tukirejelea Taksonomia ya Bloom iliyoboreshwa na Anderson na Krathwohl (2001), tunaona kwamba vitenzi vinavyotumiwa na walimu hawa wakati wa kubainisha malengo ya ujifunzaji vinaishia kwenye ngazi za chini *(eleza, fafanua).* Hivi ni vitenzi ambavyo vinamsaidia mwanafunzi kukumbuka kile alichofundishwa. Inafaa malengo haya kwenda mbele zaidi na kuonesha namna mwanafunzi atakavyofanya uchambuzi (*jadili, linganisha, linganua, tofautisha, husisha,…),* tathmini (*tathmini, linganisha, hitimisha, hakiki, tetea, thibitisha*,…) na uundaji (*panga, unganisha, tunga, tengeneza, jenga upya,* …) ili wawe na stadi ya tafakuri tunduizi. Haya yanapaswa kuzingatiwa kwa kila ngazi ya elimu kwa kuzingatia malengo ya ujifunzaji yaliyopo.

Kama inavyojitokeza kwenye ubainishaji wa malengo ya ujifunzaji, matokeo ya uchambuzi wa nyaraka za walimu yamebainisha pia kwamba walimu wa Kiswahili hawazingatii vema stadi ya tafakuri tunduizi wanapoandaa somo. Stadi hii inaonekana kwa kutajwa tu katika nafasi ya uwezo wa jumla ikiwekwa pamoja na masuala mtambuka.

Uwekaji pamoja wa tafakuri tunduizi na masuala mtambuka sio sahihi kwa sababu stadi hii inapaswa kuonekana katika uwezo wa jumla. Aidha, maelezo kadhaa yanapaswa kutolewa ili kuonesha ni namna gani stadi hii itakavyofundishwa katika somo. Suala hili pia linadhihirishwa katika utafiti wa Tuyishimire (2022).

Kimsingi, inaonekana kwamba walimu wa fasihi wanashindwa kuzingatia vema stadi ya tafakuri tunduizi wanapoandaa somo. Walimu hawa wanatumia istilahi ya *ukuzaji fikra* kwa kurejelea tafakuri tunduizi ilhali tafakuri tunduizi ni stadi ambayo ina istilahi yake mahususi. Aidha, Vdovina na Gaibisso (2013) nao wanaongeza kwamba uzingatiaji wa stadi ya tafakuri tunduizi katika andalio la somo ni changamoto kwa walimu wa lugha.

Mwongozo wa andalio la somo unaotumiwa na walimu wa Kiswahili Wilayani Nyagatare unaweza kuwapotosha kutathmini maendeleo ya wanafunzi. Hii ni kwa

sababu mwalimu hutathmini kutokana na kile alichofundisha ili ahakikishe kama malengo ya somo yamefikiwa (Alsaleh, 2020). Hivyo basi, hii ilitutia hamasa ya kuchunguza jinsi walimu wa Kiswahili wanavyoandaa tathmini za masomo yao kwa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi.

### 3.2 Tathmini ya Somo la Kiswahili kwa Kuzingatia Stadi ya Tafakuri Tunduizi

Ufundishaji wa somo lolote huendana na tathmini yake. Kwa hiyo, ni lazima wanafunzi wafanyiwe tathmini, kwani wasipotathminiwa ujifunzaji unakuwa haujakamilika. Tathmini ya kila somo inapaswa kuwasaidia wanafunzi kuhusisha kile walichosoma darasani na maisha halisi. Kwa hiyo, maswali ya tathmini yanapaswa kuwashirikisha wanafunzi kutoa hoja zao. Aidha, wanafunzi wanalazimika kutetea hoja zao kwa kutumia mifano halisi ya maisha (Vdovina na Gaibisso, 2013).

Maelezo haya yanamaanisha kwamba tathmini inapaswa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Hivyo, maswali ya tathmini ni lazima yawahamasishe wanafunzi kuunda na kutathmini hoja wanazozitoa. Aidha, wanafunzi wanapaswa kutoa mifano halisi inayohusiana na hoja zao.

Uchambuzi wa nyaraka za walimu wa Kiswahili, umebaini kwamba mitihani iliyotolewa kwa wanafunzi haikuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Data kutoka katika mitihani iliyochambuliwa zinaonesha kwamba baadhi ya maswali wanayoulizwa wanafunzi yanaishia kuwataka kurudisha kile walichojifunza darasani kuliko kuhusisha maarifa waliyopata na maisha halisi.

Katika uchambuzi wa mtihani wa muhula wa pili (2021-2022), mkazo umewekwa katika kuzingatia muundo wa mtihani wa lugha kama unavyobainishwa katika muhtasari wa somo la Kiswahili. Muhtasari huu unabainisha kwamba muundo wowote wa mtihani unapaswa kujengwa na vipengele vinne: *Ufahamu*, *Sarufi*, *Utungaji* na *Fasihi* (REB, 2015). Hivyo basi, utafiti huu ulichunguza vipengele vitatu ambavyo ni ufahamu, utungaji na fasihi. Vipengele hivi viliteuliwa kwa sababu wanafunzi wanapewa maswali yanayowalazimu kutoa hoja zao na kuzitetea kwa mifano. Maswali kama haya yanatoa fursa kwa wanafunzi kukuza stadi za tafakuri tunduizi ikiwa ni pamoja na uchambuzi, tathmini na uundaji.

Matokeo ya uchambuzi wa nyaraka za walimu yameonesha kwamba walimu wa Kiswahili hawazingatii vema stadi ya tafakuri tunduizi wanapotathmini masomo yao. Maswali ya tathmini kwa kiwango kikubwa yanawalazimu wanafunzi kurudisha kile wanachojifunza darasani kuliko kuwataka kutoa hoja na kuzitetea.

Haya yanajitokeza kwa kiwango kikubwa katika sehemu ya mbili ya mtihani (ufahamu na fasihi). Katika sehemu ya tatu ambayo ni utungaji, stadi ya tafakuri

tunduizi inazingatiwa katika tathmini. Yafuatayo ni maswali yanayotolewa katika sehemu mbalimbali za mtihani:

**Sehemu ya ufahamu**

**Jibu maswali**

1.Maana ya "mwanao ana mkono mrefu"ni:/Alama 2
a) anapenda kupigana c) Anaharibu vitu vya watu.
b) Amekuwa mwizi d) Hodari wa kurusha mikuki.

2." Nilikimbia kufiwako na nimekuja kuliwako nyama"ina maana ya:/Alama 2

a) a)Shule ya Tumaini wanafunzi huuliwa wakikosa adabu.
b) Katika shule hii wanaokosa adabu hukatiwa walete nyama kama fidia.
c) Shule ya Tumaini wanafunzi hufa kwa maradhi mengi.
d) Anatoka kubaya na kuja kubaya Zaidi.

3. Mamake Kobole alimtetea mwanawe kwa sababu:/Alama 2

a) Mwalimu wa Kobole alikuwa na chuki na mwanawe
b) Alikuwa akimlea Kobole vizuri sana.
c) Alimpenda sana Kobole
d) Mwalimu mkuu alipenda, kusikiliza walimu wake.

4. Kosa kubwa alilofanya mamake KOBOLE ni:/Alama 2

a) Kutaja utasa wa mwalimu kama adhabu kutoka kwa Mungu.
b) Kuwatisha walimu kuwapeleka maji makuu.
a) Kumhamisha Kobole kutoka shule ya Tumaini
c) Kushika kila aambiwalo kuhusu Kobole.

5.Methali gani haiwezi kutumika vizuri katika funzo la hadidhi hii./Alama 2

a) Maji yakimwagika hayazoleki c) Mpanda ovyo huvuna ovyo
b) Mwana wa nyoka ni nyoka. d ) Akipenda chongo huita kengeza.

**Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Maswali ya sehemu hii ni mazuri. Maswali haya yanaundwa kwa namna ya kuwalazimu wanafunzi kusoma kifungu cha ufahamu na kukielewa ili wajibu kwa usahihi. Hata hivyo, maswali haya hayawapi fursa wanafunzi ya kuhusisha kile wanachosoma na maisha halisi. Zaidi ya maswali haya, ingekuwa bora kuongeza maswali yanayomtaka mwanafunzi kuchambua, kutathmini na hata kuunda hoja mpya za kutetea jibu analotoa kama mtaala unavyoagiza.

Kwa mfano, wanafunzi wangetakiwa kujadili athari za kuwa na mkono mrefu kwa mtu binafsi, jamii na hata nchi kwa ujumla. Wanafunzi wangeulizwa pia ikiwa wanakubaliana na sababu zilizotolewa na mama yake Kobole za kumtetea mwanae au kutoa methali tofauti zinazohusiana na kifungu walichosoma huku wakitoa sababu za kufaa kwa methali hizo.

Kama ilivyo katika sehemu ya ufahamu, baadhi ya maswali ya sehemu ya fasihi pia hayakutungwa kwa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Maswali mawili

yanaonekana kuwataka wanafunzi kutetea hoja zao kwa mifano. Aidha, maswali mawili mengine yanaishia kwenye ngazi ya chini ya Taksonomia ya Bloom (kukumbuka na kufahamu). Hii inadhihirishwa na maswali yafuatayo waliyopewa wanafunzi:

**SEHEMU YA III: FASIHI**
**18. Eleza tabia za wahusika./Alama 5**

19. Eleza methali zifuatazo na utoe hali tunapoweza kutumia kila moja:/Alama 6
a. Patiliza udongo ungali maji
b. Kidole kimoja hakivunji chawa
c. Aliye kando haangukiwi na mti.

**20. Eleza nahau zifuatazo kisha utoe mfano wa kila moja katika sentensi:/Alama 4**
a. Kupiga marufuku
b. Kuvaa miwani

**21. Fani na Maudhui havitengani bali hutegemeana ili kazi ya kifasihi iweze kuwa bora Zaidi. Jadili/Alama 5**

**Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Maswali ya 18 na 20 ni ya msingi kwa mwanafunzi wa fasihi. Maswali haya yanamtaka mwanafunzi kukumbuka kile anachojifunza katika fasihi. Hili linathibitishwa na vitenzi vilivyotumiwa *eleza* (kukumbuka). Hivyo basi, wanafunzi watatoa maelezo kulingana na kile walichojifunza darasani. Zaidi ya maswali haya, wanafunzi wangeongezewa maswali yanayowalazimu kutetea hoja zao kwa kurejelea kazi za kifasihi walizosoma au kuhusisha nahau na maisha ya kila siku. Hili halipaswi kufanyika kwa wanafunzi wa kidato cha sita tu bali kwa wanafunzi wa viwango vingine wanaosoma fasihi.

Swali la 19 ni zuri kwa kuwa linamsaidia mwanafunzi kukuza stadi ya tafakuri tunduizi. Hii ni kwa kuwa swali hili linamtaka mwanafunzi kutoa maelezo kuhusu methali na mifano ya mazingira ambamo methali hizo zinatumiwa. Ili mwanafunzi ajibu swali hili, anatakiwa kupitia katika hatua mbalimbali za tafakuri tunduizi ambazo ni uchambuzi, tathmini na uundaji.

Swali la 21 ni zuri pia. Swali hili linamtaka mwanafunzi kufanya mjadala (*uchambuzi*). Pamoja na uzuri wa swali hili, ingekuwa bora zaidi wanafunzi wakatakiwa kutoa mifano kutoka katika kazi za kifasihi walizosoma. Maswali yangeundwa kwa namna hiyo, yangewashirikisha wanafunzi katika ujengaji hoja zinazothibitishwa na mifano kutoka kazi za kifasihi.

Vilevile, shairi lililotolewa katika mtihani lilichambuliwa. Swali lililotolewa kuhusu shairi hili linaonekana kuwa zuri kwa sababu linamtaka mwanafunzi kufanya uchambuzi. Shairi lina anwani "*Tunda*". Shairi lenyewe lina beti nane ila tulichukua ubeti mmoja kama mfano:

**22. Shairi/Alama 10**

**Tunda**

Kasha takwea mtini, nimeona bivu tunda,

Sina usone moyoni, ela tunda kasha tunda,

Nimpe wangu mwandani,jioni nishike tunda.

Meanza wao uneni,hapo name ndipo Kamba.

**Chambua shairi hili kwa kueleza na kutoa mifano kutoka shairini ya sifa za kimtindo zifuatazo:**

a. Ukwapi na Utao

b. Vina

c. Mizani

d. Kibwagizo

e. Kimalizio

f. Mishororo na beti.

**Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Swali hili linawataka wanafunzi kufanya uchambuzi. Hivyo basi, wanafunzi wanapaswa kutumia maarifa waliyoyapata darasani ili kuchambua shairi walilopewa. Pamoja na hayo, tuna mtazamo kuwa swali hili moja halitoshi. Ingekuwa bora kuweka maswali mengine yanayomtaka mwanafunzi kutumia sifa za kimtindo zinazopatikana katika shairi husika na kuendeleza shairi hili au kutunga mashairi yao.

Baada ya kujadili sehemu zinazohusika na ufahamu na fasihi, sasa tunajadili tathmini katika sehemu ya tatu. Katika karatasi ya maswali inaonekana kama sehemu ya nne inayohusika na utungaji. Kwa hakika, tathmini ya sehemu hii ipo vizuri ukilinganisha na sehemu zilizotangulia (ufahamu na fasihi). Maswali yaliyopo katika sehemu hii yanawasaidia wanafunzi kukuza stadi za tafakuri tunduizi ambazo ni uchambuzi, tathmini na uundaji.

**SEHEMU YA IV: UTUNGAJI / Alama 10**

Chagua swali mada moja kati ya hizi zifuatazo chini uandike maneno kati ya 200 na 250:

a. "Mtoto ni mtoto awe wa kike au wa kiume." Tunga insha kuonyesha ukweli wa wazo hili.

b. " Wewe ni mkuu wa idara ya utamaduni na huduma za jamii wilayani na umealikwa kuhutubia vijana kuhusu miradi yao ya kujiendeleza ." Iandike hotuba yako

**Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Ukichunguza sehemu hii ya utungaji, unaona kwamba inamtaka mwanafunzi kutunga insha au hotuba. Ili mwanafunzi atunge insha/ hotuba ni lazima akusanye hoja tofauti kuhusiana na mada yake. Aidha, mwanafunzi anahitajika kuunda na kutathmini hoja kwa ajili ya kujibu swali. Hii ina maana kwamba mwanafunzi

atahitajika kupitia hatua kadhaa za tafakuri tunduizi ikiwa ni pamoja na uchambuzi, tathmini na uundaji ili aweze kujibu swali kwa usahihi.

Kwa ujumla, data za uchambuzi wa nyaraka za walimu zilizokusanywa zinaonesha kwamba walimu wa Kiswahili wana mkanganyiko kuhusu ufundishaji na tathmini inayozingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Kwa hiyo, ni wazi kwamba wanakutana na changamoto mbalimbali katika mchakato wa ufundishaji na tathmini. Kabla ya kujadili changamoto hizo, kuna haja kwanza ya kuelewa maoni ya walimu wa Kiswahili kuhusu tafakuri tunduizi na mtaala unaoegemea katika uwezo.

### 3.3 Uelewa wa Walimu wa Kiswahili kuhusu Stadi ya Tafakuri Tunduizi na Mtaala unaoegemea katika Uwezo

Data za mahojiano zinabainisha kwamba walimu wa Kiswahili bado wana mkanganyiko kuhusu maana ya stadi ya tafakuri tunduizi. Hii inathibitishwa na majibu waliyoyatoa walipoulizwa "*Nini maana ya stadi ya tafakuri tunduizi*?"

> Stadi ya tafakuri tunduizi ni vile ambavyo mwanafunzi wa Kiswahili anavyoweza kujifunza pamoja na masomo mengine. Vitu hivyo vinaweza kumsaidia katika maisha yake ya kila siku katika utatuzi wa shida za kimaisha kama mwanajamii (mwalimu, CH).
> **Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Nukuu ya mtoataarifa huyu haibainishi wazi stadi ya tafakuri tunduizi ni nini. Ukichunguza fasili hii, unaweza kuichukulia stadi ya tafakuri tunduizi kama somo fulani, masuala mtambuka au masomo yanayoweza kutolewa kwa njia isiyo rasmi. Zaidi ya mwalimu huyu, mwalimu mwenzake kwenye shule ya D naye alionekana kutoelewa vema stadi ya tafakuri tunduizi kwa ukamilifu wake. Mwalimu huyu alisema kwamba:

> Stadi ya tafakuri tunduizi ni kama namna ya kuwafundisha wanafunzi. Mwanafunzi unampa kidogo na kumuomba mengi. Mwanafunzi ni lazima atumie uwezo wake wa kufikiri kwa kazi anayopewa. Kwa mfano, mwanafunzi unaweza kumpa maana ya fasihi kisha naye akatafuta maarifa mengine kuhusu fasihi (mwalimu, D).
>
> **Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Mtoataarifa huyu anaichukulia stadi ya tafakuri tunduizi kama mbinu ya ufundishaji ambapo mwanafunzi unampa maarifa machache na kumuomba mengi. Hivyo, mwanafunzi unaweza kumpa utangulizi wa somo naye akaendelea mpaka mwisho wa somo. Ingawa maelezo hayo yana ukweli, lakini si ukweli kamili. Tunakubaliana kwamba mwanafunzi anapaswa kushiriki kikamilifu katika ujengaji wa maarifa kama baadhi ya mihimili ya Nadharia ya Ujengaji inavyobainisha, lakini mwanafunzi anahitaji mwongozo wa mwalimu kwa kila hatua.

Madondoo ya watoataarifa hawa wawili ni ithibati kwamba walimu wa Kiswahili hawaelewi vema stadi ya tafakuri tunduizi. Tatizo hili limebainishwa pia na Tuyishimire (2022). Mtafiti huyu amebaini kwamba walimu wa Kiswahili Wilayani Nyarugenge bado hawajaielewa vema stadi ya tafakuri tunduizi.

Fasili za walimu hawa kuhusu stadi ya tafakuri tunduizi zinatufanya kujiuliza kama wana uelewa wowote kuhusu mtaala unaoegemea katika uwezo. Hii inatokana na kwamba stadi ya tafakuri tunduizi inafanikisha utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo (Tuyishimire, 2022). Hivyo basi, hatuwezi kuzungumzia tafakuri tunduizi na kusahau mtaala unaoegemea katika uwezo.

Data za mahojiano pia zimebainisha kwamba walimu wa Kiswahili hawaelewi vema mtaala unaoegemea katika uwezo. Haya ni baadhi ya maoni ya walimu kwenye shule za B na D walipoulizwa: *"Nini maana ya mtaala unaoegemea katika uwezo?"*

> Mtaala unaoegemea katika uwezo ni uwezo wa mwanafunzi katika kutenda jambo kwa masomo anayojifunza. Na hivyo tunaangalia jinsi wanafunzi wanavyojifunza, nguvu zao na jinsi wanavyofikiri kwa kuangalia mchango wa somo na kile litakachomsaidia (mwalimu, B).
>
> **Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Mtoataarifa huyu anafafanua mtaala unaoegemea katika uwezo kama uwezo wa mwanafunzi kufanya jambo fulani kutokana na kile alichojifunza. Mtaala unaoegemea katika uwezo haumaanishi uwezo wa mwanafunzi bali unajikita katika ukuzaji wa uwezo wa mwanafunzi. Mwanafunzi anapaswa kushirikishwa katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kumsaidia kuhusisha darasa na maisha halisi ya utatuzi wa tatizo. Hoja hii pia inatetewa na mojawapo ya mihimili ya Nadharia ya Ujengaji unaosema kwamba ujifunzaji wa utatuzi wa tatizo unapaswa kuwa lengo kuu la ujifunzaji.

Licha ya mwalimu huyu kutoka shule B, mwalimu mwenzake kutoka shule D naye anaonekana kutoelewa vema mtaala unaoegemea katika uwezo. Mwalimu huyu anaufafanua mtaala unaoegemea katika uwezo ifuatavyo:

> Mtaala unaoegemea kwenye uwezo ni mtaala mamboleo, unaoegemea kwenye ujuzi wa mwanafunzi kuliko ujuzi wa mwalimu, yaani mwanafunzi anapewa nafasi kubwa. Maana kwamba mtaala ambao unampa mwanafunzi muda wa kutosha katika kujifunza (mwalimu, D).
>
> **Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Nukuu ya mtoataarifa huyu inamaanisha kwamba mtaala unaoegemea katika uwezo unajikita kwenye ujuzi wa mwanafunzi kwa kupewa nafasi kubwa lakini haoneshi kazi ya mwalimu katika utekelezaji wa mtaala ni ipi. Pili, fasili yake haioneshi kiasi gani cha muda wanachopewa wanafunzi katika mchakato wa

ufundishaji. Inaonekana kama vile mwalimu anatoa maarifa machache kwa wanafunzi kisha wao wakashughulika na kazi inayobaki.

Madondoo ya watoataarifa hawa ni ithibati kwamba walimu wa Kiswahili bado hawajaelewa mtaala unaoegemea katika uwezo kwa ukamilifu wake. Shida hii pia imethibitishwa na Mukashema (2022). Mtafiti huyu anaonesha kwamba walimu wa Kiswahili wilayani Nyamagabe, nchini Rwanda wana changamoto ya kufasili mtaala unaoegemea katika uwezo.

### 3.4 Changamoto za Kufundisha na Kutathmini Stadi ya Tafakuri Tunduizi

Matokeo ya mahojiano yameonesha kwamba walimu wa Kiswahili wanakutana na changamoto tofautitofauti katika ufundishaji na tathmini inayozingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Changamoto ya kwanza inayowakabili walimu wa Kiswahili ni ukosefu wa uelewa wa kina kuhusu stadi ya tafakuri tunduizi. Changamoto hii kwanza inajitokeza kupitia mahojiano yao na mtafiti. Aidha, changamoto hii ilithibitishwa na mmojawapo wa walimu kwenye shule (A):

> Kuna changamoto nyingi ambazo zinawakabili walimu wa Kiswahili. Kwanza kuna walimu ambao hawajui stadi ya tafakuri tunduizi ni nini. Kutokana na kutoielewa, wanapata changamoto kuifundisha vilivyo kwa kila somo. Na hivyo hawawezi kutathmini kile ambacho hawakufundisha (mwalimu, A).
>
> **Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Dondoo hili linaonesha kwamba walimu wa Kiswahili wanashindwa kufundisha na kufanya tathmni inayozingatia stadi ya tafakuri tunduizi kwa sababu ya ukosefu wa maarifa kuhusu stadi hii. Hii inatokana na ukweli kwamba walimu wengi hawakuandaliwa katika mazingira yanayowasaidia kuwa na stadi hii (Snyder na Snyder, 2008). Aidha, hakuna programu zinazowasaidia walimu wa lugha kujifunza zaidi kuhusu tafakuri tunduizi (Bataineh na Alazzi, 2009).

Maelezo haya yanaonesha kwamba misingi mibaya ya walimu wa lugha kikiwamo Kiswahili kuhusu stadi ya tafakuri tunduizi inaathiri namna ya kufundisha na kutathmini somo kwa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi kwa upande mmoja. Kwa upande mwingine, walimu wa Kiswahili hawana mafunzo toshelevu kuhusu utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo ambao msingi wake ni tafakuri tunduizi. Hili linathibitishwa na walimu wote walioshiriki katika utafiti huu.

Katika utafiti wake, Nsengimana (2021) anasema kwamba 20.5% tu ya walimu ndio walipata mafunzo kuhusu utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo katika Wilaya ya Muhanga, nchini Rwanda. Mafunzo haya mara nyingi yalitolewa kwa lugha ya Kiingereza. Kwa hiyo, walimu wa Kiswahili hawakupata mafunzo haya kwa lugha ya wanayofundisha.

Hivyo basi, mafunzo ni muhimu kwa walimu wa Kiswahili kwa sababu ni mojawapo ya mahitaji ya ufundishaji wa tafakuri tunduizi. Aidha, Paulsen (2022) anasisitiza hili kwa kusema kwamba mafunzo kwa walimu ni muhimu kuliko kuwa na mtaala unaoweka mkazo kwenye tafakuri tunduizi. Hivyo, mtaala unaoweka mkazo kwenye stadi ya tafakuri tunduizi unahitaji walimu waliopata mafunzo.

Changamoto ya pili ni ukosefu wa vifaa vya kufundishia. Walimu wote wa Kiswahili walioshiriki katika utafiti huu walisema kwamba wanatatizika na upataji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Huyu ni mmojawapo wa walimu hao:

> Sisi kama walimu wa Kiswahili tuna shida kubwa ya ukosefu wa vifaa vya kufundisha ikiwemo vitabu vinavyohusu mtaala unaoegemea katika uwezo. Kwa mfano, mimi ninafundisha Kiswahili kutoka kidato cha nne hadi cha sita, ila nina kitabu kimoja kwa kila kidato. Hii ina maana kwamba mwanafunzi anamaliza mwaka bila kupata fursa ya kusoma kitabu (mwalimu, CH).
> **Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Dondoo hili linaonesha kwamba walimu wa Kiswahili hawana vitabu vya kutosha wanavyoweza kuvitumia katika ufundishaji. Walimu hawa waliendelea kusema kwamba hawana pia vitabu vya kusoma kama vile riwaya au hadithi fupi. Mwalimu mmojawapo, akieleza kuhusu changamoto hii alisema kama ifuatavyo:

> Wanafunzi wanaojifunza lugha ya Kiswahili wanahitaji pia kazi za kifasihi za kusoma. Hii inatokana na kwamba ni vigumu kufundisha fasihi bila vitabu vya kusoma. Vitabu vya Kiswahili vinavyoandaliwa kwa ajili ya kutumiwa katika ufundishaji haviwezi pekee kuwasaidia wanafunzi kujifunza fasihi kwa ukamilifu (mwalimu, D).
> **Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Madondoo haya mawili yanaonesha kwamba walimu wa Kiswahili wana changamoto ya ukosefu wa vitabu vya kutumia katika ufundishaji na ujifunzaji. Matokeo yake ni kushindwa kufundisha vilivyo. Changamoto hii pia inathibitishwa na utafiti wa Tuyishimire (2022). Matokeo ya utafiti wake yanathibitisha kwamba walimu wengi wa Kiswahili hawana vifaa vya kutosha ikiwa ni pamoja na vitabu vya fasihi. Hivyo basi, walimu wa Kiswahili wanapaswa wapatiwe vifaa vya mbalimbali vya kufundisha ikiwa ni pamoja na vitabu vya fasihi. Hii ni kwa sababu mojawapo ya masharti ya kufundisha tafakuri tunduizi ni pamoja kuwapo kwa vifaa vya kufundishia (Mashaza, 2017).

Aidha, inapendekezwa kwamba wakati walimu wa Kiswahili wanaposubiri serikali kutoa vifaa (vitabu), wanaweza kuazima vitabu vya kutumia katika shule jirani. Hii inatokana na ukweli kwamba kuna baadhi ya shule za sekondari ambazo zina vitabu vingi kuliko shule nyingine. Viongozi wa shule pia wanaweza kuwasaidia walimu kupiga hatua na kutengeneza vifaa vyao wenyewe kwa kiwango cha shule.

Changamoto ya tatu ni uwezo mdogo wa wanafunzi wa kuwa na umilisi wa lugha lengwa. Data za mahojiano na walimu zimeonesha kwamba wanafunzi hawana umilisi wa lugha ya Kiswahili kutokana na kukosa msamiati wa kutosha. Athari yake ni kwamba wanashindwa kujieleza na kueleza hoja zao wanapofanya mijadala kuhusu mada mbalimbali. Jambo hili lilithibitishwa na mmojawapo wa walengwa wa utafiti kama ifuatavyo:

> Wakati mwingine, kuna pia wanafunzi wa Kiswahili ambao hawana uwezo wa kujieleza katika Kiswahili kwa sababu hawana msamiati wa kutosha. Mwanafunzi ana hoja nyingi za kutetea msimamo wake ila anashindwa kupata msamiati sahihi wa kutumia. Mara nyingi wanafunzi wa Kiswahili wanashindwa kujibu maswali kwa usahihi kwa sababu ya uhaba msamiati (mwalimu, B).
>
> **Chanzo:** Data za Utafiti (2022)

Dondoo hili linaonesha kwamba kutokuwa na umilisi wa lugha ya Kiswahili ni kikwazo kwa wanafunzi cha kuwa na stadi ya tafakuri tunduizi. Hivyo, wanafunzi wenye umilisi wa lugha lengwa wanabahatika kuwa na tafakuri tunduizi kutokana na kujieleza kwa urahisi kimaandishi na kimazungumzo (Indah na Kusuma, 2016).

Hivyo basi, inapendekezwa kwamba walimu wanapaswa kuwashirikisha wanafunzi katika usomaji/ usikilizaji wa kazi mbalimbali za kifasihi kama vile hadithi, riwaya na nyimbo. Hii itawasaidia kwanza kuwa na tafakuri tunduizi kutokana na kile ambacho watapata katika kazi husika. Pili ni kukuza msamiati wa Kiswahili na hatimaye kupata kichocheo cha kutunga kazi zao wenyewe.

Utungaji wa kazi kama hizi utatoa fursa kwa wanafunzi kujiajiri na kutatua shida ya ukosefu wa kazi za kifasihi zinazoweza kutumiwa katika ufundishaji. Hii inathibitishwa na mmojawapo wa mhimili wa Nadharia ya Ujengaji usemao kwamba utatuzi wa tatizo unapaswa kuwa moyo wa ujifunzaji.

## 4.0 Hitimisho

Makala haya yalikusudia kujadili ufundishaji na tathmini inayozingatia stadi ya tafakuri tunduizi kwa masomo ya Kiswahili miongoni mwa shule teule za sekondari katika Wilaya ya Nyagatare, nchini Rwanda. Jambo kubwa tulilobaini katika mjadala huu ni kwamba walimu wa Kiswahili wanashindwa kufundisha na kutathmini kwa ukamilifu masomo wanayofundisha kwa kuzingatia stadi ya tafakuri tunduizi. Jambo hili linatokana na kutumia malengo ya ujifunzaji ya kiwango cha chini katika Taksonomia ya Bloom na kuuliza maswali ambayo yanamtaka mwanafunzi kukariri kile alichosoma badala ya kukihusisha na hali halisi ya maisha. Makala yanabainisha kuwa dosari hii inatokana na changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu: kukosa uelewa kuhusu stadi ya tafakuri tunduizi, ukosefu wa mafunzo ya utekelezaji wa mtaala unaoegemea uwezo, uhaba wa vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji, na kiwango cha chini cha lugha miongoni mwa wanafunzi.

Pamoja na hayo, makala yanatoa mapendekezo ya kukabiliana na changamoto hii: kutoa mafunzo ya mara kwa mara ya utekelezaji wa mtaala unaoegemea katika uwezo, kutumia mbinu mwafaka za ufundishaji lugha na kujitengenezea vifaa vya ufundishaji na ujifunzaji. Aidha, makala yanapendekeza kufanyika kwa tafiti zaidi kuhusu ufundishaji na tathmini inayozingatia stadi ya tafakuri tunduizi kwa kujikita katika viwango mbalimbali vya elimu.

**Marejeleo**

Alsaleh, N. J. (2020) "Teaching Critical Thinking Skills". *The Turkish Online Journal of Educational Technology*, Juz. 19 (1): 21–39. Inapatikana katika https://doi.org/10.4324/9780429342042. Ilisomwa tarehe 10 Septemba 2022.

Anderson, L. W. na Krathwohl, D. A. (2001) *Taxonomy for Learning, Teaching, and Assessing: A Revision of Bloom's Taxonomy of Educational Objectives*. Boston: Pearson Education Group.

Bakhshandeh, B. (2021) *Perception of 21st Century 4Cs (Critical Thinking, Communication, Creativity na Collaboration) Skills Gap in Private-Sector Employers in Lackawanna County, Nepa*. Tasinifu Uzamivu. (Haijachapishwa). Pennsylvania State: Chuo Kikuu cha Pennsylvania. Inapatikana katika https://rb.gy/khqeyo. Ilisomwa tarehe 6 Juni 2022.

Bataineh, O., na Alazzi, K. F. (2009) "Perceptions of Jordanian Secondary Schools Teachers towards Critical Thinking". *International Education.* Juz. 38 (2): 56-72.

Carrasco, N. (2021) "*English Teachers and their Understanding of Critical Thinking. A Submitted Degree Project in School of Education, Culture and Communication"*. Stockholm: Chuo Kikuu cha Malardalen. Inapatikana katika https://rb.gy/wgtjhg. Ilisomwa tarehe 7 Septemba 2022.

Chu, S. K. W., Reynolds, R.B., Tavares, N.J., Notari, M., Lee, C.W.Y. (2017) "21st Century Skills and Global Education Roadmaps". *Spinger Science*, Juz. 7(17): 1-14. Inapatikana katika https://doi.org/10.1007/978-981-10-2481-8_2. Ilisomwa tarehe 6 Juni 2020.

Cresswell, J. W. (2012) *Educational Research: Planning, Conducting, and Evaluating Quantitative and Qualitative Research* (Toleo la 4). New York: Pearson.

Ertmer, P. A. na Newby, T. J. (2013) "Behaviourism, Cognitivism, Constructivism: Comparing Critical Features from an Instructional Design Perspective". *Performance Improvement Quarterly,* Juz. Na. 6 (2): 43-71.

Iakovos, T. (2011) "Critical and Creative Thinking in the English Language Classroom". *International Journal of Humanities and Social Science*, Juz. 1 (8): 82-86.

Indah, R. N., na Kusuma, A. W. (2016) "Factors Affecting the Development of Critical Thinking of Indonesian Learners of English Language". *Journal of Humanities and Social Science,* Juz. Na. 21(6): 86-94.

Kaufman, J. K. (2013) "21 Ways to 21st Century Skills: Why Students Need Them and Ideas for Practical Implementation". *Kappa Delta Pi Record*, Juz. Na. *9*(2): 78-83.

Khalid, L. Bucheerei, J. na Issah, M. (2021) "Pre-Service Teachers' Perceptions of Barriers to Promoting Critical Thinking Skills in the Classroom". *SAGE Open,* Juz.Na. 11 (3): 1-9.

Lau, F. Y. J. (2011) *An Introduction to Critical Thinking and Creativity*: *Think More, Think Better.* Canada: A John Wiley na Sons Publication.

Masduqi, H. (2011) "Critical Thinking Skills and Meaning in English Language Teaching". *Teflin Journal*, Juz. Na. 22 (2):185-200.

Mashaza, L. G. (2017) "Theoretical Perspectives on Critical Thinking Teaching: Reflections from Field Experiences from a Norwegian Lower Secondary School in Comparison to Tanzanian Secondary School Teaching Practices". *Journal of Education and Learning,* Juz. Na. 11(3): 312-318.

Mukashema, C. (2022) *Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kusoma na Kuandika kwa Wanafunzi wa Kiswahili wa Shule za Sekondari Wilayani Nyamagabe.* Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Rwanda, Kigali.

Muraraneza, C. Mtshali, N. G. na Mukamana, D. (2017) "Issues and Challenges of Curriculum Reform to Competency Based Curricula in Africa: A Meta-Synthesis". *Nursing and Health Sciences*, Juz. 19(1): 5-12.

Ndihokubwayo, K. Habiyaremye, H. T. na Rukundo, J. C. (2019) "Rwandan New Competence based Curriculum implementation and Issues sector-based Trainers. LWATI": *A Journal of Contemporary Research,* Juz. 16(1): 24-41. Inapatikana katika https://files.eric.ed.gov/fulltext/ED595372.pdf. Ilisomwa tarehe 15 Machi 2023.

Nsengimana, V. (2021) "Implementation of Competence-based Curriculum in Rwanda: Opportunities and Challenges". *Rwandan Journal of Education,* Juz.Na. 5(1): 129-138.

Olusegun, S. (2015) "Constructivism Learning Theory: A paradigm for Teaching and Learning". *Journal of Research & Method in Education*, Juz. Na. 5(6), 66-70.

Paulsen, V. H. (2022) *Challenging Aspects of Critical Thinking: A Mixed-methods Study of Students' Test Results, Students' Reasoning, and Teaching Strategies*.Tasinifu ya Uzamivu (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Bergen, Bergen. Inapatikana katika https://rb.gy/sj3bi0. Ilisomwa tarehe 9 Septemba 2023

REB. (2015) *Muhtasari wa Somo la Kiswahili Kidato cha 4-6: Mchepuo wa Lugha.* Kigali: REB.

REB. (2015a) *Teacher Training Manual: Roll out of the Competence-Based Curriculum*. Kigali: REB.

Schendel, R. (2015) “Critical Thinking at Rwanda's Public Universities: Emerging Evidence of a Crucial Development Priority”. *International Journal of Educational Development*, Juz. Na. 4(1): 1–16. Inapatikana katika https://doi.org/10.1016/j.ijedudev.2015.04.003 Ilisomwa tarehe 12 Novemba 2022.

Snyder, L. G. na Snyder, M. J. (2008) “Teaching Critical Thinking and Problem Solving Skills”. *The Journal of Research in Business Education*, Juz. Na. *50*(2): 90-99.

Sulaiman, L. N. (2012) *Incorporating Critical Thinking: Teaching Strategies In Malaysian Technical And Vocational Education (TVE) Programs.* Tasinifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Colorado State, Colorado. Inapatikana katika https://rb.gy/zv78rm. Ilisomwa tarehe.22 Julai 2022.

Sünbül, M. A. na Kurnaz, A. (2016) “Critical Thinking and How to Teach Critical Thinking Skills”. Katika Kaya, Z. na Akdemir, S. (Wah.) *Learning and teaching: Theories, Approaches and Models* (Toleo la 2). Ankara: Çözüm Publishing. Kur.174-193.

Tuyishimire, L. (2022) *Ukuzaji wa Stadi ya Tafakuri Tunduizi kupitia Ufundishaji wa Fasihi: Mfano wa Shule Teule za Sekondari Wilayani Nyarugenge.* Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Kigali: Chuo Kikuu cha Rwanda.

Vdovina, E. na Gaibisso, L. C. (2013). “Developing Critical Thinking in the English Language Classroom: A Lesson Plan”. *Elta Journal*, Juz. Na. 1(1): 54-68. Inapatikana https://www.academia.edu/7816264/Developing_Critical_Thinking_in_the_English_Language_Classroom. Ilisomwa tarehe 22 Juni 2022.